



RASILIMALI ZA SERA

Sera: Kufunga Maombi Yaliyotelekezwa katika Usimamizi wa BRC

Tarehe ya Kuanza: Februari 1, 2024

Kiungo cha Sera: <https://www.mass.gov/doc/eec-closing-abandoned-requests-in-brc-manager-policy-documentswahili/download>

Iwapo wewe au wafanyakazi wako mna maswali kuhusu sera hii au mnahitaji usaidizi wa ziada, tafadhali wasiliana na Kituo cha Mawasiliano cha EEC katika 617-988-7841.

Maswali na Majibu kuhusu wa Maombi ya BRC Yaliyotelekezwa au Yasiyokamilika

1. Ombi la BRC likifungwa itamaanisha nini? Je, uamuzi wa ufaafu hufanywa?

Hakuna uamuzi wa ufaafu unaofanywa wakati ombi la BRC limefungwa kwa sababu zilizotajwa katika sera hii. Ombi la BRC hufungwa tu katika mfumo wa Usimamizi wa BRC.

2. Je, maombi ya BRC yenye masharti na ya kusasishwa yatafungwa?

Ndiyo. Kufungwa kwa maombi ya BRC kutaathiri waombaji waliopo katika hali yenye masharti na/au kusasishwa ikiwa watakosa kuchukuliwa alama zao za vidole ndani ya siku 120.

3. Je, ikiwa mwombaji amekuwa na matatizo ya kuchukuliwa alama za vidole (k.m., matatizo na IdentoGO)?

Ikiwa mwombaji kwa sasa anawasiliana na EEC kuhusu suala ambalo limemzuia kuchuliwa alama za vidole kati ya siku 120, ombi lake la BRC halitafungwa. Zaidi ya hayo, ikiwa mwombaji ana miadi ya kuchukuliwa alama za vidole iliyoratibiwa kufanyika tarehe ya baadaye, ombi lake la BRC halitafungwa. Iwapo mwombaji anakumbana na changamoto za kuchukuliwa alama za vidole, anafaa kupiga simu kwa Kituo cha Mawasiliano cha EEC katika 617- 988- 7841.

4. Je, ikiwa mwombaji ambaye BRC imefungwa kwa sasa anafanya kazi katika mpango?

Mwombaji anayefanya kazi kwa sasa katika mpango ambaye ombi lake la BRC limefungwa lazima aondolewe kwenye mpango wake wa sasa ndani ya siku 14. Hakuna mwombaji aliye na BRC isiyokamilika au iliyofungwa anayeweza kufanya kazi katika mpango hadi atakapopatikana kuwa Anafaa.

5. Je, iwapo mwombaji aliye na BRC-iliyofungwa bado angependa kuajiriwa?

Ikiwa mwombaji anataka kuendelea na mchakato wa BRC baada ya ombi lake lililotelekezwa kufungwa, mpango unaweza kuwasilisha fomu mpya ya idhini iliyotiwa saini kutoka kwa mwombaji. Mwombaji atahitaji kuingizwa katika Tovuti ya Mpango wa Kielekezi cha BRC kama “Wasilisho Jipya” la mpango. Ni lazima jina la mwombaji liandikwe jinsi linavyoonekana kwenye kitambulisho chao cha picha.